**TANGAZO LA SERIKALI Na. …………………….. la Tarehe ………………………..**
**SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

---

**SURA YA 290**

---

**SHERIA NDOGO**

---

**Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(2) na 16(1)**

# SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI WILAYA YA BUTIAMA YA BUTIAMA ZA MWAKA, 2025

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi ziitwe Sheria Ndogo za afya na usafi wa mzingira za Halmashauri ya Wilaya ya Butiama za Mwaka 2025 na zitaanza kutumika mara baada ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi ispokuwa kama itaelezwa vinginevyo, tafsiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-

Sura 290

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa hii ni pamoja-

(a) Kitu chochote kinachotumika katika matengenzo ya chakula
(b) Kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula
(c) Kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula mfano binzari

"Mkazi" maana yake ni mtu yeyote anaishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri

"Choo chakuvuta" maana yake ni choo ambacho kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na tanki ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi mahali palipoandaliwa

"Choo cha Umma" maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma

''Afisa Mwidhiniwa'' maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhiniwa kutekeleza chochote chini ya Sheria Ndogo hizi;

''Halmashauri'' maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Butiama;

”Eneo la wazi“ maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa

”Hati ya usafi” maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

”Huduma” maana yake ni shuguhuli zote zinatotolewa na Halmashauri au mtu mwingine yeyote ambazo zinapaswa kulipiwa ada kwa mujibu wa sheria ndogo.

‘‘Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na itajumuisha Kaimu Mkurugenzi;

’’Soko’’ Maana yake ni sehemu au eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua bidhaa na mazao.

”Jengo la biashara”maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa.

”Mmiliki maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote katika Kijiji endapo mazingira husika ni Kijiji au barabara za vitongoji.

”Kaya” maana yake ni jumla ya watu ambao kwa kawaida huishi na kula pamoja kwa kushirikiana katika kupata mahitaji yao ya kila siku.

Kituo cha taka maana yake ni kizimba cha taka(point of collection) kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri

‘’’Mwenyekiti’ maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri;

“Maji taka’’ maana yake ni kama ilivyo katika sheria ya mazingira 2024 ni pamoja taka zinazotokana na kinyesi mkojo na jasho uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi majengo ya biashara na viwanda

”Mazao au mime mirefu” maana yake ni mazao au mimea inayozidi sentimenta 15 kwenda juu kama vile mtama mihogo mahindi, mbaazi uwele na mengine yote yale yanayofanana.

”Mzalishaji wa taka ngumu” maana yake ni mtu yeyote au taasisi , kaya, biashara , kiwanda ambaye katika kutekekeleza shughuli zake huzalisha taka

”Pipa” maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani sehemu za biashara maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira

”Taka” kama ilivyo katika sheria ya usimamizi wa mazingira 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi,na mionzi kinachotoa

harufu mbaya au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo uozo au hali nyingine inayosababisha uharibifu wa mzingira ambayo inajumuisha taka.

”Taka ngumu” ni kama ilivyo katika sheria ya usimamizi wa mazingira 2004 ni taka ambazo haziko katika majimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara , viwanda na kutoka katika shughuli za kilimo pamoja na taka za vyakula, karatasi, plastic au taka laini zinatokana na ujenzi au ubomoaji wa majengo na utengenezaji wa bustani na shughuli za uchimbaji madini mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu(scrap).

”Taka za Majumbani” maana yake itajumuisha mabaki ya chakula ,maganda ya matunda ,majivu kinyesi cha mifugo taka za bustani,marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbali mbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa.

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:

”Taka Viwandani” kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya usimamizi na mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiyotokana na uzalishaji wa viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyoitiwa dawa au pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyo tafsiriwa katika sheria ya usimamizi wa mazingira 2004 sehemu ya IX.

“Mwaka wa fedha” maana yake ni Mwaka wa Fedha kama unavyotambuliwa Serikali;

“Choo bora” maana yake ni choo chochote chenye kuta na sakafu inayosafishika kwa maji, banda imara la kudumu,lililoezekwa, lenye mlango imara,choo chenye kutumika wakati wote wa majira. salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi,

”Taka hatarishi” kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya mazingira Na 20 ya mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kigumu ,chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, hospitalini, au mafuta machafu ambayo yanaleta Athari za kikemia kwa binadamu au mazingira.

”Wakala” maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu ,kampuni, taasisi, au shirika aliyeteuliwa kisimamia utekelezaji wa sheria ndgo hizi.

”Vyakula vya kupikwa au kukaangwa” maana yake ni nyama,wali,ndizi ,ugali maandazi vitumbua mikate samaki chipsi ,kuku na vinginevyo

”Ufugaji wa ndani” maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya eneo lililoruhusiwa tu.

”Uchunguzi wa Afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vimelea vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi.

## SEHEMU YA PILI
## USAFI WA MAZINGIRA

**Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira**

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabishara anaye miliki eneo la nyumba kuhakisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanazonguka makazi au eneo lake la kazi kwa kuhakikisha kwamba.

(a) Majani yanayozunguka nyumba au makazi yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya biashara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake.

(b) Takataka zitakusanywa , kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwawa na Halmashauri au mamlaka husika.

(c) Kuwa na pipa au chombo cha kutunzia taka kwa muda kabla ya kupelekwa dampo.

**Ushiriki wa wananchi katika kufanya usafi wa mazingira**

5. (1) Kutakuwa na siku maalum ambayo Halmashauri itatenga kwa lengo la wananchi kufanya usafi kuanzia saa 1.00 asubuhi hadi saa 3.00 asubuhi na biashara zote zitafungwa wakati wa zoezi la usafi likifanyika

**Wajibu wa kulipa Ada/ushuru**

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kwamba anashiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku maalum kila mwezi zilizopangwa na Halmashauri na mwananchi atakayekata kushiriki katika shughuli za kufanya usafi atakuwa ametenda kosa.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara

**Mimea mirefu Mjini**

6. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo mjini pamoja na maeneo mengine yatakayozuiliwa na Halmashauri;

**Usafi wa mifeji au mitaro ya maji ya mvua**

7. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga majani nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya kiwanja cha nyumba yake au eneo la biashara yake kiwanja chake na kuhakiksha mfereji au mtaro huo unakuwa msafi na imara siku zote.

**Taa za nje ya nyumba**

8. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

**Kupaka rangi na anwani za makazi katika majengo**

9. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anapaka rangi na kuweka namba ya anwani ya makazi kwenye nyumba yake au duka lake au jengo lake la biashara;

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu | 10. | | Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji machafu takataka au kitu chochote cha maji au kuhakisha kuwa vyombo vya maji au matanki au visima vyote vimefunikwa au makopo au chupa za plastiki au vifuu vyote vinavyoweza kutunza maji maji vinaondolewa katika eneo lake la kuishi au la biashara. |
| Biashara ya matunda na mboga mboga | 11. | (1) | Itakuwa ni ni wajibu wa kila mfanyabishara ya matunda au mboga mboga kuhakisha kuwa ana chombo maalum cha kuweka au kuhifadhi maganda au mabaki ya matunda au mbogamboga. |
| | | (2) | Ni marufuk mtu yeyote kufanya biashara ya matunda au mboga mboga au biashara nyingine yeyote katika maeneo yasiyoruhusiwa |
| Upulizaji dawa | 12. | | Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yeyote au mahali popote bila kuwa na cheti au kibali cha taasisi husika ya serikali au lesseni kutoka Halmashauri. |
| Matengenezo ya magari pikipiki na mitambo | 13. | (1) | Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yanatakiwa kufanyika kwenye karakana,gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri. |
| | | (2) | Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa. |
| | | (3) | Ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha gari kwenye chanzo chochote cha maji au karibu na chanzo hicho kunakosababisha chanzo cha maji hayo kuchafuliwa au kwenye mifereji au mitaro ya maji ya mvua au maeneo ya wazi ambayo hayajatengwa kwa kazi hiyo au barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo. |

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA VYAKULA

| | | | |
|---|---|---|---|
| Usalama wa maji ya kunywa | 14. | | Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anachemsha maji na kuchuja maji yote yanayotumika kwa kunywa ili kuyafanya yawe safi na salama bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji. |
| Utengenezaji na uuzaji vilivyokuwa | 15. | (1) | Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza kuchoma, kupima au kuuza chakula cha aina yeyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka Halmashauri. |

**Uuzwaji wa vyakula vilivyopikwa**

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vyakupikwa au kukaangwa kuhakisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lilotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini.

(a) Vyakula vyote vinatakiwa kuwekwa juu ya meza

(b) Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate,nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kupima afya yake kila baada ya miezi sita na atalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi 5000/=

(c) Mmiliki yeyote atakaye ruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atawajibika kulipa faini isiyozidi tsh 50,000/=.

**Usimamizi wa Vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko**

16. Afisa mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula pombe mikusanyiko sherehe yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti maandishi au kuptia vyombo vya habari au mikutano ya ya hadhara endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta Athari za maisha ya binadamu.

**Machinjio na maduka ya nyama**

17. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakisha kwamba duka lake

(a) Ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu, lina maji safi,magogo na misumeno ya kukatia nyama.

(b) Lina kabati ya vio na jokofu la kuhifadhiwa nyama sehemu za kuweka mizani

(c) Kuna pipa la kuifadhia takataka

(d) Muuzaji ana vazi jeupe pamoja na apron nyeupe

(e) Muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita.

**Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa**

18. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyo kuwa na machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwana Halmashauri.

**Ufugaji wa wanyama**

19. (a) Itakuwa ni marukufu kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani barabarani au kuchungwa kwenye eneo la taasisi au eneo lolote lisiloruhisiwa

(b) Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakisha kwamba.- Anakusanya uchafu wowote utokanao na wanyama kama vile kinyesi manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupwa kwenye dampo au kupelekwa shambani kama mbolea

Uwezo wa kukagua

20. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi kukagua utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

Afisa Mwidiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halikaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti yaliyotolewa katika sheria ndogo hizi .

## SEHEMU YA NNE
## USIMAMIZI WA TAKA TAKA

Wajibu wa Halmashauri

21. (1) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka dampo na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji hadi kwenye dampo, Isipokuwa mmiliki wa kiwanda atakuwa na wajibu wa kuzoa taka zitakazozalishwa katika kiwanda chake na kuzitupa katika eneo lililotengwa(dampo).

(2) Kwamba Halmashauri itakuwa na jukumu la kuingia mikataba na makumpuni yaliyosajiliwa au Taasisi au kuhamasisha uundaji wa vikundi jamii (CBOS) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika maeneo yake baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

22. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangaji, mfanyabiashara au taasisi kuhakikisha kuwa ana chombo chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia taka ngumu kabla ya kupelekwa kwenye kizimba au kuchukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakisha kwamba anatupa uchafu , maganda ya matunda, mabaki ya vocha za simu , vifungashio vya bidhaa au chupa tupu za maji au soda katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutuzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka au uchafu wowote au kuacha kuwepo takatka au uchafu kwenye nyumba uchochoroni ,kiwanja, mfereji wa maji ya mvua barabara na maeneo ya nyumban au mahali popote ambapo hapajatengwa kwa shughuli hiyo.

Uhifadhi majitaka

23. Kila mmiliki wa nyumba au taasisi anatakiwa kuhakisha kuwa ana karo la kuhifadhia maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutirisha maji taka | 24. | | Ni marufuku kumwaga au kutirisha au kuelekeza maji taka kutoka vyooni bafuni,karoni au jengo lolote la biashara baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda babarani ,uchochoroni,mtoni kwenye vyanzo vya maji maeneo ya wazi mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka hayo.Endapo hali hiyo ya katazo itabainika kuwepo mmiliki au mpangaji atalipa faini ya Tsh 50,000 au kifungo cha miezi mitatu au vyote viwili. |
| Uendeshaji wa viwanda | 25. | | Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana mashine ya kusaga, kuranda mbao kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli nyingine yeyote ya kiwanda inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi au mipango miji. |
| | 26. | | Kwamba endapo mmiliki wa kiwanda cha madini ya dhahabu au mengine atatirisha maji yenye sumu katika eneo la makazi na akasababisha hasara kwa wananchi au pasipo kusababisha hasara atawajibika kulipa faini tsh 500,000/= au kifungo cha miezi 12 au vyote kwa pamoja. |
| Ada za uzoaji taka | 27. | (1) | Halmashauri itatoza ada ya uzoaji wa taka kwa viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi. |
| | | (2) | Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na ada zote zitakusanywa kwa kutumia mfumo uliokubalika na serikali wa mashine za POS toka kwa afisa mwidhiniwa wa Halmashauri. |
| | | (3) | Bila kuathiri kifungu 27(1) ada ya uzoaji wa taka itajulikana kama tozo ya usimamizi wa taka kwa wamiliki wa viwanda au mzalishaji wa taka kutoka majumbani au eneo la biashara au viwandani. |
| | | (4) | Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji wa taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kumfikishwa mahakamani. |
| Uteuzi wa wakala | 28. | | Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi cha jamii au mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya sheria ndogo hizi. |

## SEHEMU YA TANO
## UJENZI NA MATUMIZI YA CHOO.

| | | |
|---|---|---|
| Wajibu wa kuwa na choo na kutumia | 29. | Itakuwa ni wajibu wa kila mtu au mpangaji wa nyumba au Taasisi kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi ,imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba au Taasisi hiyo na kuhakisha kinatumika wakati wote. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Umbali wa Choo | 30. | | Choo kinatakiwa kujengwa umbali wa mita sitini (60). Kutoka kwenye kisima au kwenye chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya binadamu au nyumbani |
| Vyoo vya Umma | 31. | (1) | Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi,vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma(Public Toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo. |
| | | (2) | Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmshauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyoelekezwa na Halmashhauri katika mkataba wake na mawakala watakaopewa jukumu la kusimamia vyoo hivyo. |
| Vyoo vya muda katika mikusanyiko | 32. | | Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye jengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kilichojengwa itawazimu wahusika wa eneo hilo kujenga choo cha muda kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri. |
| Vyoo katika majengo ya biashara | 33. | | Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya sheria ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya jinsia za kike na kiume. |
| Ilani ya kujenga choo | 34. | (1) | Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Midhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akianisha masharti ya kurekebisha hali hiyo. |
| Kufungwa kwa jengo la biashara | | (2) | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 32(1) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa. |
| Ilani ya kuondoa kero | 35. | (1) | Endapo afisa Mwidiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji au mtumiaji au mtu yeyote anyehusika akimtaka kuondoa kero hiyo. |
| | | (2) | Mtu atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioanishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa katika sheria ndogo hizi na akipatikana na hatia anatakiwa kulipa faini ya tsh50,000/=. |
| Mkurugenzi kuteua Mkaguzi | 36 | 3. | Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri |

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

| | | | |
|---|---|---|---|
| Makosa ya jumla | 37 | (1) | Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo.<br>(a) Atamzuia au kujaribu kumzuia afisa Mwidiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya sheria ndogo hizi.<br>(b) Atamsawishi mtu au kundi la watu kumzuia |

mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya sheria ndogo hizi.

(c) Atamwaga takataka katika mtaro wa maji ya mvua uchochoroni au mahali popote hadhrani au katika eneo la wazi bila idhini ya Halmashauri

(d) Ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi.

(e) Atatirisha au kumwaga maji machafu barabarani au katika eneo la wazi au la nyumba ya jirani

(f) Ataosha magari kufua kunywesha mifugo na kukoroga dawa za kuulia wadudu ndani mito mabwabwa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu

(g) Atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo ambayo yametengwa kwa ajili ya kuuza pasipo kufuata taratibu za afya

(h) Atafanya matengenezo ya magari ,pikipiki na mitambo kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli izo bila kuzingatia taratibu za mipango miji.

(i) Atatiririsha maji ya sumu kutoka katika vinu vya uchenjuaji au kiwandani au sehemu anayofanyia uzalishaji na kuingia katika makazi ya watu au sehemu isiyokuwa na makazi ya watu

(j) Ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi.

(k) Ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani uchochoroni upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni

(l) Atashindwa kujenga choo katika makazi au katka eneo alolifanyia biashara

(m) Atashindwa kuweka vyombo vya uchafu katika eneo la biashara.

(n) Atasindwa kuhifadhi chakula kwenye Kabati safi lililofunikwa na lenye kioo.

Adhabu 38. Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya tsh 200,000/= au isiyozid tsh 900,000/=au kifungo cha miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

## SEHEMU SABA
## JINSI YA KUCHUKUWA HATUA KWA MTU ALIYEKIUKA SHERIA NDOGO HIZI

Uwezo wa kumuita mtu aliyekiuka sera

39. Mkurugenzi anaweza kumuita mtu yeyote afike mbele yake au mbele ya Afisa muidhiniwa kwa muda unaofaa na kutoa maelezo yanayohitajika kuhusiana na kukiuka sheria ndogo hizi.

Uwezo wa Mkurugenzi kufifilisha kosa

40. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mlipa ushuru au mtu aliyetenda kosa, chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mlipa ushuru huyo amekiri kwa maandishi kwa Mkurugenzi, kuwa ametenda kosa hilo na kuwa atalipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini na kisha atapatiwa stakabadhi ya malipo hayo.

Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji

41. (1) Kwamba Mkurugenzi Mtendaji anaweza kupunguza kiasi cha ushuru kiliachoanishwa kwenye sheria ndogo hizi na kuruhusu kiasi pungufu kilipwe na mlipaji au kisilipwe kutokana na sababu atakazoziona yeye zinafaa baada ya kuashauriana na Mwenyekiti wa Halmashauri.

Kufungua Shauri Mahakamani

42. Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 37 na Sheria Ndogo ya 38, endapo mlipa ushuru au mtu yeyote atashindwa kulipa ushuru au adhabu, Halmashauri itafungua shauri la madai kwa njia ya mkato [summary procedure] katika Mahakama yenye uwezo wa kusikiliza shauri hilo.

Hati ya Kukamata Mali

43. (1) Bila ya kuathiri Sheria ndogo ya 37,38 na 39, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri,kukamata mali ya mtu ambaye atakiwa kulipa ushuru lakini hajalipa au ametozwa faini lakini hakulipa kwa wakati.

(2) Hati atakayopewa mlipa ushuru na Mahakama itakuwa na mamlaka ya kisheria ya kukamata na kuuza mali inayoondosheka ya Mlipa ushuru au mtu aliyekiuka sheria ndogo hizi na kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa nia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hizi, itakuwa ni uthibitisho kamili wa maelezo ya madai yaliyoelezwa chini ya hati hiyo.

**JEDWALI**

_ *(Limetungwachiniyakifungucha29)*

**ADA YA UZOAJI WATAKA**

| NA | AINA YA MAKAZI/BIASHARA | NDANI YA MAENEO YA MIJI MIDOGO | NJE YA MIJI MIDOGO |
|---|---|---|---|
| 1. | Baa au Club ya usiku | 2,000/ | 1,000/ |
| 2. | Bucha | 1,500/= | 800/= |
| 3. | Nyumba za kuishi(kwa kaya) | 500/= | 200/= |
| 4. | Watengeneza juice au barafu au bisi | 1,000/= | 300/= |
| 5. | Mgaha wa midogo/mamalishe n.k | 2,000/= | 1,000/= |
| 6. | Migahawa(Café,Restaurant n.k) | 2500/= | 1,500/= |
| 6. | Wachoma,chips,nyama, kuku, Mahindi na mihogo | 25,00/= | 1,000/= |
| 7. | Zahanati za watu Binafsi | Ajenge kichomea taka au alipe 10,000/ | Ajenge kichomea taka au alipe 8,000/ |
| 8. | Vituo vya afya vya watu binafsi | 5 Ajenge kichomea taka au alipe 50,0000,000/= | Ajenge kichomea taka au alipe 30,000 |
| 9. | Hospitali za watu binafsi | Ajenge kichomea taka au alipe 80,000/= | Ajenge kichomea taka au alipe 50,000/= |
| 10 | Groceries | 2,500/= | 1,500/= |
| 11. | Maduka ya madawa | 2,000/= | 1,500/= |
| 13 | Vizimba au Vioski au meza za biashara | 1,000/= | 500/= |
| 14. | Mafundi seremara au fanicha na magereji | 3,000/= | 2,000/= |
| 15. | Wachomelea vyuma na vyuma chakavu | 2,000/= | 1500/= |
| 16. | Karakana na waosha magari, pikipiki na bajaji. | 2,000/= | 1,500/= |
| 17. | Vyuo/shule za binafsi za Bweni | 3,000/= | 2,500/= |
| 18. | Vyuo/shule za binafsi za kutwa | 1,000/= | 8,00/= |
| 19. | Maduka ya jumla | 2,000/= | 1,500/= |
| 20. | Maduka ya rejareja | 1,500/= | 1,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21. | Magari yanayo shusha mizigo kwenye masoko kwa tripu | 3,000/= kwa siku | 1,000/= |
| 22. | Magari yanayoshusha mizigo sehemu za nje ya soko kwa tripu | 2,000/= | 1,000/= |
| 23. | Boti inayoshusha mizigo/abiria mwaloni kwa safari | 1,000/= | 1,000/= |
| 25. | Vilabu vya wauza pombe za kienyeji | 1,500/= | 1,000/= |
| 26. | Saloon | 1500/= | 1,000/= |
| 27. | Nyumba za kulala wageni | 3,000/= | 1,500/= |
| 28. | Wauza mkaa wa jumla na rejareja | 1,500/= | 1,000/= |
| 29. | Maduka ya vitabu na viandikia internet café | 1,500/= | 1,000/= |
| 30. | Maduka ya vifaa vya ujenzi | 2,000/= | 1,500/= |
| 31. | Vituo vya mafuta | 2,000/= | 1,500/= |
| 32. | Mashine ya kusaga nafaka | 1,500/= | 1000/= |
| 33. | Mashine ya kukoboa nafaka | 5,000/= kwe mwezi | 3,000/= |
| 34. | Wauza mbao | 1,000/= | 800/= |
| 35. | Karakana za kuranda mbao | 3,000/= | 2,000/= |
| 36. | Ofisi za binafsi | 800/= | 500/= |
| 37. | Mafundi baiskeli | 800/= | 500/= |
| 38. | Wauza Mitumba | 1,000/= | 500/= |
| 39. | Wauza mitumba nje ya soko | 500/= | 200/= |
| 40. | Wauza nafaka | 2,000/= | 1,000/= |
| 41. | Waziba pancha mitaani | 800/= | 500/= |
| 42. | Wafuga kuku, bata, kanga n.k kwenye vizimba | 1,000/= | 800/= |
| 44. | Wauza samaki sokoni | 1,000/= | 1,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 45. | Wauza natunda mboga mboga na viungo sokoni au nje ya soko | 1,000/= | 500/= |
| 46. | Viwanda vya kukamua mafuta ya kupikia | 2,000/= | 1,500/= |
| 47. | Wauza maji, togwa, soda nje na ndani ya soko | 1,000/= | 800/= |
| 48. | Hoteli | 2,000/= | 1,500/= |
| 49. | Taasisi za kifedha | 1,000/= | 1,000/= |
| 50. | Vibanda vya Airtel,Vodacom,Tigo,Halo tel n.k (Money Transfer) | 1,000/= | 1,000/= |
| 51. | Taasisi zingine au biashara zingine ambazo hazijatajwa hapa | 2,000/= | 2,000/= |
| 52. | Pumba za mbao kwa trip<br>-4.5m$^3$<br>-6m$^3$<br>-10m$^3$ | <br>6,000.00/=<br>10,000.00/=<br>15,000.00/= | <br>6,000.00/=<br>10,000.00/=<br>15,000.00/= |
| 53. | Viwanda vidogo kwa trip<br>-4.5m3<br>-6m3<br>-10m3 | <br>8,000.00/=<br>12,000.00/=<br>15,000.00/= | <br>8,000.00/=<br>12,000.00/=<br>15,000.00/= |
| 54. | Maegesho ya malori au Tipper .<br>**i. chini ya masaa6**<br>-Lori chini yatani 7<br>-Lori kuanzia tani7nazaidi<br>**ii. zaidi ya masaa6**<br>-Lori chini ya tani 7<br>-Lori kuanzia tani7 na zaidi | <br><br>2,000.00/=<br>3,000.00/=<br><br>3,000.00/=<br>5,000.00/= | <br><br>2,000.00/=<br>3,000.00/=<br><br>3,000.00/=<br>5,000.00/= |
| 55. | Ada ya kutupa taka katika dampo kuu kwa siku kwa mtu binafsi<br>-Lori chini ya tani7<br>-Lori tani 7na zaidi | <br>10,000.00/=<br>30,000.00/= | <br>20,000.00/=<br>30,000.00/= |
| 56. | Usafirishaji wa taka rejeshi(Recycling) kwa safari | 20,000.00/= | 20,000.00/= |

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya vibandikwe katika SheriaNdogo hizi kwa ajili ya udhibitisho kwa matumizi ya kila siku.

……………………………                                   ……………

*Peter W. Nyerere*
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
***Halmashauri ya wilaya ya Butiama.***

*Aziza J. baruti*
*MkurugenziMtendaji (W),*
***Halmashauri yawilaya ya Butiama***

,

**NAKUBALI: leo tarehe……………………mwezi ……………………….……….2025**

*……………………………*
*Mohamed Mchengerwa,*
*WAZIRI OR*
*TAMISEMI,*